FOMU PLUPA L-2 (r.10)

**JAMHURI YA KENYA**
**SHERIA YA MPANGO WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI**
**(*Nambari* 13 *ya* 2019)**

# ILALNI KUHUSU KUKAMILISHWA KWA MPANGO WA USTAWISHAJI

Kichwa cha Mpango wa Ustawishaji:
**Kurasimishwa kwa Mahala pa Kutekelezwa kwa Mpango wa Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu eneo la Milimani, Manisipaa ya Kakamega, Kaunti ya Kakamega.**
**Nambari ya PDP: NRB/16/2025/01**
**ILANI** inatolewa kwamba, kwa mujibu wa hitaji la Sehemu za 13(g), na 69(1) ya Sheria ya Mpango wa Miji na Mpango wa Matumizi ya Ardhi, 2019 ikisomwa pamoja na Notisi ya Sheria Nambari 27 ya 2020, utayarishaji wa mpango uliotajwa hapo juu ulikamilika mnamo Februari 11, 2025.
Mpango huo wa Ustawishaji unahusu ardhi iliyoko katika mji wa Majengo, kaunti ya Vihiga.
Nakala za Mpango huo wa Ustawishaji ulivyotayarishwa umehifadhiwa kwa ukaguzi na umma, bila malipo, katika Afisi za **Kamishna wa Kaunti ya Kakamega**,**WAZIRI WA KAUNTI Anayesimamia Idara ya Mpango wa Miji na Matumizi ya Ardhi-Kaunti ya Kakamega** na **Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji-Orofa ya 5 Jumba la Ardhi House, Nairobi; kati ya saa mbili za asubuhi (8.00 am) na saa kumi na moja jioni (5.pm), Jumatatu hadi Ijumaa.**
Mtu yeyote ambaye angetaka kutoa maoni au pingamizi kuhusu Mpango wa Ustawishaji uliotajwa hapo juu anaweza kuziwasilisha, kwa maandishi, ili zipokelewe na Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji, barabara ya 1st Ngong' Avenue, Jumba la Ardhi House, S.L.P. 45025-00100, Nairobi au zitumwe kwa njia ya barua pepe: ndpp@ardhi.go.ke ndani ya siku sitini (60) baada ya kuchapishwa kwa ilani hii. Na maoni au pingamizi hizo sharti ziandamanishwe na sababu zilizochangia kutolewa kwazo..
**TAREHE**: Machi 7, 2025.

Dkt. Peris Mang'ira, PhD, HSC
**MKURUGENZI WA KITAIFA WA IDARA YA MPANGO WA MIJI.**